TANGAZO LA SERIKALI NA. 378 la tarehe 15/5/2020

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA. 290)

## SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA MAZAO YA MAJINI (MAREKEBISHO) YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME YA MWAKA 2020

Jina la sheria

Tangazo la Serikali Na 95 la Mwaka 2011

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Majini (Marekebisho) ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2020 na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Mazao ya Majini) ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2011 ambazo katika Sheria Ndogo hii zitajulikana kama "Sheria Ndogo Kuu"

Marekebi-sho ya kifungu cha 7

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta Kifungu cha 7 na badala yake kuweka Kifungu kipya kama ifuatavyo:

"7. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya sheria Ndogo hii atapewa adhabu ya faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja".

Marekebi-sho ya Jedwali la Kwanza

3. Sheria Ndogo Kuu inafanyiwa marekebisho kwa kufuta Jedwali la Kwanza na badala yake kuweka Jedwali la kwanza la sheria ndogo hii:

"JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 4.)*

ADA NA USHURU WA KUSAFIRISHA SAMAKI

| Na. | Aina ya Ada na Ushuru | Kiwango cha Ada na Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa kusafirisha samaki | 10,000/= kwa kila safari |
| 2. | Leseni ya kufanya biashara ya samaki | 20,000/= kwa mwaka |
| 3. | Ushuru wa kono la samaki | 10,000/= kwa siku" |

Marekebisho ya Jedwali la Pili

4. Sheria Ndogo kuu inafanyiwa marekebisho kwa kufuta Jedwali la Pili na badala yake kuweka Jedwali la Pili la Sheria ndogo hii.

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya Kifungu cha 5.)*

ADA YA KUANDIKISHA VYOMBO VYA UVUVI

| Na. | Aina ya Ada | Kiwango cha Ada |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya usajili wa vyombo vya uvuvi | 30,000/= kwa mwaka |
| 2. | Kubadili jina la chombo cha zamani | 5,000/= kila kinapobadilishwa |

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Same umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuatia Azimio lililopitishwa na mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 29/3/2019.

ANNA CLAIRE SHIJA
*Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Same*

CHRISTOPHER M. IRIRA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,Same*

NAKUBALI,

L.S

*Dodoma,*
16 Aprili, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB.),
*WN OR-TAMISEMI*
*Dodoma*